JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA | WIZARA YA KATIBA NA SHERIA

# SHERIA BULLETIN

Toleo la Saba

# MAMA SAMIA LEGAL AID CAMPAIGN SHINYANGA

MAMA SAMIA Legal Aid Campaign

## ZUIO LA NDOA YA MWANAFUNZI



## YALIYOMO


03 | MSLAC yamkomboa binti aliyekatisha masomo Shinyanga

05 | Shinyanga yaandamwa na Ukatili wa Kijinsia

08 | Msaada wa kisheria kutolewa bure kila Jumamosi ya Mwisho wa Mwezi



## BODI YA UHARIRI

**MARY MAKONDO**
Katibu Mkuu

**LUSAJO MWAKABUKU**
Kaimu Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini

**WAJUMBE**
George Mollel | William Mabusi | George Mwakyembe | Felix Chakila

**Wasanifu wa Kurasa:** Waziri Bosco | Richard Mwamakafu


CS CamScanner




# SHINYANGA YAAHIDI USHIRIKIANO KATIKA UTEKELEZAJI WA MAMA SAMIA LEGAL AID CAMPAIGN.

**Na Lusajo Mwakabuku & William Mabusi – WKS Shinyanga**

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga Mhe. Christina Mndeme ameiahidi Wizara ya Katiba na Sheria na wadau inaoshirikiana nao katika kuendesha kampeni ya kitaifa ya msaada wa kisheria - Mama Samia Legal Aid Campaign kutoa ushirikiano wa hali na mali katika kufikia malengo ya kampeni hii ya kutoa msaada wa kisheria kwa watanzania wote hasa wale waishio maeneo ya pembezoni huku akiagiza kata zote zihakikishe zinanatenga maeneo maalum ambayo watoa huduma wataweza kuongea na mwananchi mmoja mmoja kwa faragha.

Mheshimiwa Mndeme alitoa kauli hiyo alipokuwa akihutubia kabla ya kuzindua rasmi utekelezaji wa kampeni hiyo mkoani Shinyanga hafla iliyofanyika katika viwanja vya Sabasaba Shinyanga mjini leo tarehe 11/06/2023 huku akiwaalika wakazi wote wa mkoa wa Shinyanga kushiriki Mama Samia Legal Aid Campaign itakayotolewa bure kwa wanachi katika Halmashauri zote sita kuanzia tarehe 11 - 21 Juni, 2023.

"Kwa mara nyingine tena, ninatoa wito kwamba sisi sote tushikamane katika kumuunga mkono Kiongozi wetu, Mama yetu, Mlezi wetu na Mtetezi wa Wananchi hususan wanyonge Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassani, Rais wa Jamhuri wa Muungano wa Tanzania katika kuondoa kadhia na viashiria vyote vya kuminya upatikanaji wa haki hususan ukatili wa Kijinsia kwa Wanawake na Watoto ambayo ndiyo changamoto kubwa ya Mkoa wa Shinyanga". Alisema Mhe. Mndeme

Itaendelea....



*Mgeni Rasmi katika Uzinduzi wa utekelezaji wa Mama Samia Legal Aid Campaign (MSLAC) na Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga Mhe. Christina Mndeme akisoma hotuba ya ufunguzi katika hafla hiyo iliyofanyika katika viwanja vya Sabasaba tarehe 11/06/2023.*



*Meza kuu wakipita katika mabanda yanayotoa huduma wakikagua kazi zinazofanywa na wataalam wanaoendesha kampeni hii ya msaada wa kisheria MSLAC*



CamScanner

Inaendelea ...

Mkuu wa Mkoa huyo aliongeza kuwa kampeni hii inatukumbusha watanzania wote uwajibikaji na usimamizi wa maamuzi yenye kuleta haki na akatumia fursa hiyo kuwambusha watumishi wote kutojihusisha na masuala ya rushwa inayopelekea kuzorotesha upatikanaji haki. Aidha Mhe. Mndeme alimuahidi Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa katika utekelezwaji wa Kampeni hii kwa kipindi cha miaka mitatu, ofisi yake itasimamia maadili kwa lengo la kuboresha upatikanaji wa haki kwa usawa.

Akitoa salaam na kumkaribisha Mgeni Rasmi, Naibu Waziri wa Wizara ya Katiba na Sheria Mhe. Pauline Gekul amesema Wizara itaendelea kushirikiana na Mikoa yote ya Tanzania Bara na Zanzibar kuhakikisha Kampeni hiyo inatekelezwa ipasavyo ili kuwafikia watanzania kwenye Kata na Mitaa yote nchini.

Mhe. Gekul amesema Wizara ya Katiba na Sheria inamshukuru Mhe. Rais kwa kuendelea kudumisha utawala wa sheria; uzingatiwaji wa haki za binadamu na watu na kuimarisha upatikanaji wa haki kwa wananchi wote lakini kwa jicho la kipekee kwa wananchi wasiokuwa na uwezo.

"Huduma ya msaada wa kisheria kuwafikia wananchi bure ni mapenzi na upendo mkubwa wa Mhe. Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mwananchi wa hali ya chini," alisema Mhe. Gekul.

Akitoa maelezo ya awali kuhusu Mama Samia Legal Aid Campaign, Katibu Mkuu wa Katiba na Sheria Bi. Mary Makondo ametaja mafanikio ya kampeni hii toka ilipozinduliwa Mkoani Dodoma na kuendelea katika mkoa wa Manyara kuwa ni pamoja na kusuluhishwa kwa migogoro mingi ya kijamii na hata kifamilia iliyohusu ardhi iliyodumu miaka minne, mitano, na mwingine miaka kumi kulikopelekea watu hawa ambao walikuwa hawasalimiani na hata hawazikani kumaliza tofauti zao.

"Ziko familia ambazo wanafamilia walikuwa hawaongei kutokana na migogoro inayohusiana na ardhi, mirathi na sasa wamesuluhishwa katika Kampeni na wameungana katika kujenga familia zao na taifa kwa ujumla." alisema Bi. Makondo.

Aidha Bi. Makondo amesema kwa kuwa kuna uwezekano mazingira ya mikoa hiyo kuwa sawa na Shinyanga hivyo uzoefu wa utatuzi wa migogoro hiyo utasaidia Kampeni hiyo kushughulikia masuala yote ya ukatili wa kijinsia, migogoro ya ardhi, mirathi na wosia na kuelimisha jamii kuhusu haki na wajibu wao wa kisheria na kikatiba kwa mbinu na uzoefu uliopatikana mikoa iliyotangulia na hivyo kuwezesha kampeni hiyo kufanyika kwa mafanikio makubwa zaidi katika mkoa wa Shinyanga.

Umuhimu wa kampeni hii ni wa kipekee katika kuongeza wigo wa ufikiwaji haki kwa wananchi, hususan walio vijijini na ambao hawawezi kumudu gharama za mawakili. Kampeni hii pia imekuwa msingi mzuri wa kujenga uelewa wa wananchi kuhusu haki zao za kikatiba na kisheria; jambo ambalo ni muhimu katika kulinda na kukuza haki za binadamu nchini. Hii ni kampeni ya miaka mitatu yenye lengo la kufikia mikoa yote nchini huku ikitarajiwa kuhitimishwa mwaka 2026.



*Naibu Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Pauline Gekul (Mb) akiongea na wananchi wa Shinyanga katika Hafla hiyo ya uzinduzi wa utekelezaji wa Mama Samia Legal Aid Campaign Mkoani Shinyanga*



*Katibu Mkuu wa Katiba na Sheria Bi. Mary Makondo akitoa maelezo ya awali juu ya utekelezaji wa Mama Samia Legal Aid Campaign Mkoani Shinyanga.*



*Bi. Jane Matinde akimwakilisha Makamu Mwenyekiti wa Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia – MSLAC katika ya uzinduzi wa utekelezaji wa kampeni hiyo Mkoani Shinyanga.*



*Meza kuu wakipita katika mabanda yanayotoa huduma wakikagua kazi zinazofanywa na wataalam wanaoendesha kampeni hii ya msaada wa kisheria MSLAC*



CS CamScanner

# MAMA SAMIA LEGAL AID CAMPAIN YAMKOMBOA BINTI ALIYEKATISHWA MASOMO SHINYANGA



*Askari wakiwaamrisha maharusi kuondoka katika enea la sherehe na kuingia katika magari tayari kwa safari ya kuelekea kituo cha polisi.*

## Na. George Mwakyembe – WKS

Kampeni ya Mama Samia Legal Aid inayondelea mkoani Shinyanga imendelea kuleta matunda chanya baada ya watalaam wa Mama Samia Legal Aid Campaign wakiambatana na Mkuu wa Mkoa huo Bi. Christina Mndeme na vyombo vya ulinzi na usalama kupinga kufungwa kwa ndoa iliyomhusisha binti ambaye amechaguliwa kuingia kidato cha tano katika Sekondari ya Urambo mkoani Tabora. Binti huyo mwenye umri wa miaka 19 amemaliza sekondari ya Mwawaza Mkoani Shinyanga na kupata alama daraja tatu ponti 22 na akafanikiwa kuchaguliwa kuendelea na masomo ya kidato cha tano na sita.

Lakini pasipo kujali matarajio ya ndoto zake za baadae wazazi wa binti huyu wakamua kumuozesha na kupata mahali ya ng'ombe 13 pamoja na pesa taslimu kiasi cha shilingi laki tatu. Moja kati ya maono ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kufikia hatua ambayo vitendo vya ukatili wa kijinsia dhidi Watoto na wanawake pamoja na vitendo vya unyanyasaji ambavyo vimekuwa vikiongezeka katika jamii zetu vinatokomezwa. Kitendo cha kumkatisha masomo mtoto wa kike ni kitendo cha kumyima haki ya kupata elimu na ni kitendo cha ukatili wa kijinisia sababu nyingine iliyoifanya timu ya wataalam hawa wakiambatana na Mkuu wa Mkoa kutega mtego uliofanikisha kudhibiti suala hili.

Akiongea na Wananchi waliohudhulia sherehe hiyo Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga Bi. Christina Mdeme amesema "Vitendo Kama hivi havikubaliki kwenye jamii zetu, tuwaache watoto wasome ili watimize ndoto za maisha yao lazima wazazi tuwalinde watoto wetu kwa kuwasimamia vizuri ili watimize ndo za maisha yao na si kuwakatishia ndoto zao.

Mndeme aliongeza kwamba mwanafunzi huyo ambaye amemaliza kidato cha nne katika Shule ya Sekondari Mwawaza mwaka jana na kuchaguliwa kuendelea na kidato cha tano mwaka huu wazazi wake walitaka kukatisha ndoto zake kwa kumuozesha bila ridhaa yake.



*Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga Bi. Christina Mndeme akiongea na wananchi wa Kijiji cha Mwawaza juu ya athari za ndoa za utotoni*

Mndeme amesema kitendo hicho hakiwezi kuvumiliwa kwani kinasababisha watoto wa kike washindwe kufikia malengo yao waliyojiwekea kutokana na tamaa za baadhi ya wazazi ambao wanataka kupata mali kwa haraka jambo ambalo haliwezi kuvumiliwa na Serikali pamoja na jamii.

"Tukiwa katika utekelezaji wa kampeni ya huduma ya msaada wa sheria ya Mama Samia tukapata taarifa za mwanafunzi anaozeshwa na wazazi wake wameshapokea mahali siku nyingi, tukaweka mtego na kufanikiwa kuwakamata wakiwa katika harusi hiyo, nitoe rai kwenu wananchi vitendo hivi vikome, waacheni watoto watimize malengo yao na siyo kutumia nguvu kudhurumu haki yao kwa kuwaozesha kwa nguvu" alisema Mndeme.

John Shija, ambaye ni mratibu wa Mama Samia Legal Aid Campaign kutoka shirika la Paseshi linalojihusisha na msaada wa kisheria amelaani kitendo hicho akidai kimewasikitisha kwani Serikali inaweka mazingira mazuri ya watoto kusoma lakini bado kuna baadhi ya wazazi wanakuwa kikwazo.

Mama Samia Legal Aid Campain imetekelezwa mkoani Shinyanga katika Wilaya zote za mkoa huo ambapo ilianza kutolewa kuanzia tarehe tarehe 11- 21 Juni 2023.



*Maharusi wakiwa chini ya ulinzi kuelekeo kituoni.*



CamScanner

# MSLAC YAMSAIDIA MJANE KUKABIDHIWA KIWANJA CHAKE KILICHOVAMIWA.



**Na George Mollel & Lusajo Mwakabuku**

Habari ya mgogoro wa ardhi katika eneo la Ibinzamata Manispaa ya Shinyanga ulioripotiwa toka timu ya MSLAC ilipotia nanga katika mkoa huu umefikia tamati tarehe 16/06/2023 baada ya timu ya MSLAC kwa kushirikiana uongozi wa mkoa na vyombo vya ulinzi na usalama kutekeleza amri ya mahakama iliyompa ushindi Bi. Fatuma Maganga (Mjane) ambaye ni mama wa kijana Frank Daudi aliyerithi kiwanja hicho kutoka kwa mume wake.

Mgogoro huo umetokana na uvamizi wa eneo ambalo Bi. Fatuma Maganga ambaye ni mama wa kijana Frank Daudi aliyerithi kiwanja hicho kutoka kwa mume wake. Hata hivyo Bi Fatuma hakuweza kutumia eneo hili baada ya kuvamiwa na Ndg Nyakato Sadiki ambaye aliendeleza na hatimaye kuweka uzio eneo lote la mjane huyu.

Mgogoro huu umeendelea katika vyombo vya haki kuanzia baraza la ardhi, nyumba na makazi kisha rufaa na mapitio kwenye ngazi ya mahakama kuu. kwa muda wa miaka 11 Mjane huyu amekuwa akingaika kutafuta haki yake na hatimaye mahakama kuu kupitia maombi ya mapitio mwaka 2017 iliamuru Mjane huyu arudishiwe eneo lake, na serikali isimamie utekelezaji na mama huyu kupata haki.

Kutokana na kukosa uelewa, hofu na unyonge kwa alivevamia eneo lake ambaye hakuwa tayari kukabidhi eneo hilo licha ya kuwepo kwa amri halali ya mahakama, Bi Fatuma alifika katika viwanja vya sabasaba kuomba kampeni ya MSLAC iingilie kati na kumsaidia kupata haki yake. Maafisa na timu ya kampeni iliratibu zoezi hili ikiwa ni pamoja na kupata nyaraka zote muhimu na kukutana na mlalamikiwa na kufanya mazungumzo ili aweze kurudisha eneo hilo kwa njia za amani.

Hatahivyo aliyevamia alikaidi kuondoka na kutishia kurudi mahakamani kupinga utekelezaji wa amri ya mahakama. Baada ya majadiliano ya amani kushindikana, timu ya MSLAC kwa kushirikiana na ofisi ya RC, Manispaa, Vyombo vya dola walifanikiwa kuvunja uzio na nyumba alizoweka mvamizi katika eneo la mjane na kumkabidhi mjane huyo eneo lake likiwa salama. Pamoja na makabidhiano huku mvamizi alionywa kutombugudhi mjane huyo.



Ikumbukwe kuwa lengo kuu la kuanzisha kampeni hii, pamoja na kuwasaidia wanyonge ni kupinga ukatili unaofanywa kwa wanawake wanyonge wasio na uwezo kutumia nguvu kudai haki zao. Mjane huyu amekatiliwa haki ya kumiliki mali na kujipatia kipato ambacho kingemsaidia na familia yake kwa muda mrefu swala lililowafanya wataalam hawa kuweka mkazo katika kuhakikisha suala hili haki inapatikana.

Aidha kwa Kupitia MSLAC, Mgogoro uliodumu kwa miaka 30 umefanikiwa kufikia tamati kati ya
Bw Magoso Ezekiel anayemiliki kihalali kiwanja No. 59 na Bw Nyakato Sadiki ambaye ndie aliyevamia eneo la mjane ambaye yeye anayemiliki kiwanja No. 58 eneo la ibinzamata, Shinyanga ambao wamedumu kwenye Mgogoro huu kuanzia mwaka 1993. Baada ya kusikia uwepo wa kampeni ya MSLAC bwana Magoso alifikisha malalamiko yake juu ya bwana Nyakato kuvamia eneo lake na kuweka nyumba ambayo imedumu kwa miaka mingi hivyo kumyima haki kufurahia eneo lake analomiliki kihalali. Baada ya malalamiko hayo kuifikia timu ya MSLAC walikutana na mlalamikiwa na kummweleza athari za uvamizi nah atua zitakazochukuliwa.

Majira ya jioni ya Tarehe 16/06/23, timu ya kampeni iliwakutanisha mlalamikaji na mlalamikiwa na kujadili mustakabali wa mgogoro huo. Hatimaye baada ya majadiliano ya muda, pande zote mbili zilikubaliana kumaliza mgogoiro huu kwa njia ya amani.

Katika makubaliano hayo, bwana Nyakato (mlalamikiwa) alikubali kuachia nyumba yake iliyojengwa kwenye eneo la bwana Magoso (mlalamikaji) kuanzia tarehe 16/06/202 na pia kuanzia tarehe 16/06/23 baada ya utekelezaji wa masharti haya, Mgogoro huu utakuwa umeisha na Ndg Magoso hataendelea na mgogoro huu katika vyombo vya dola.

Makubaliano mengine ni pamoja na bwana Nyakato kujenga ukuta mpya wa kutenganisha eneo lake na eneo la bwana Magoso na kwamba kwa ajili ya Utu, Ubinadamu na ujirani mwema bwana Magoso Ezekiel atamkabidhi bwana Nyakato Sadiki kiasi cha Shs 2,300,000 kama kifuta jasho kwa nyiumba atakayoachiwa na bwana Nyakato.

Makabidhiano hayo yamefanyika katika eneo la tukio tarehe 17/06/23 ambapo mlalamikaji bwana Magoso, mlalamikiwa bwana Nyakato, Shahidi wa makubaliano ambye ni mke wa mvamizi pamoja na ssuluhishi wameweka Saini kwenye makubaliano haya.





CS CamScanner

# SHINYANGA BADO YAANDAMWA NA UKATILI WA KIJINSIA



Mratibu wa timu ya wataalam kutoka Wizara ya Katiba na Sheria iliyofika kata ya Kolandoto bwana George Mollel akitoa elimu ya sheria kwa wanakijiji cha Mwagunguli.


**Na Lusajo Mwakabuku – WKS Shinyanga**


Mkoa wa Shinyanga umetajwa kuendelea kukabiliwa na matukio ya ukatili wa kijinsia ikiwemo vipigo, mimba na mauaji na sababu kuu ikitajwa kuwa ni jamii kuendelea kushikiria mila na desturi zilizopitwa na wakati, elimu ndogo pamoja na jamii kutokuwa tayari kutoa taarifa ya matukio hayo.

Afisa ustawi wa jamii wa Hospitali ya Mkoa wa Shinyanga ambaye ni mmoja wa wataalam wanaoetekeleza Mama Samia Legal Aid Campaign (MSLAC) mkoani humo, bwana Leopold Hamza aliyasema hayo wakatiakititoa elimu ya kijinsia wakati timu hiyo ya wataalam ilipokutana na wananchi wa vijiji vya Mwamagunguli na Galamba vya kata ya Kolandoto mkoani Shiyanga ambapo elimu mbalimbali za kisheria pamoja na msaada wa kisheria vilitolewa kwa wananchi hao tarehe 14/06/2023.

Afisa Ustawi wa Jamii huyo alisema bado changamoto za ukatili ni tatizo ikiwemo ukatili wa utumikishwaji wa watoto katika shughuli mbalimbali zikiwemo katika mashambani ya tumbaku, migodi midogo na majumbani, masuala ya ubakaji na ulawiti, mimba za utotoni zinazokatisha ndoto za watoto pasipo kujali sheria ya mtoto ya mwaka 2009 na ile ya ajira.

"Kinachosikitisha zaidi ni kwamba jamii inawafahamu wakosaji na mara nyingine kuwalinda kwa kuamua kumalizia kesi nyumbani au kutotoa taarifa mapema wanapoona vitendo vya ukatili. Hali hii hutoa mwanya kwa watuhumiwa kurudia vitendo hivyo mpaka siku inayopelekea kifo. Hii inaleta madhara makubwa zaidi na hata kifo, pia inarudisha nyuma maendeleo ya nchi na juhudi za serikali katika kuleta maendeleo na kufikia usawa wa kijinsia na maendeleo endelevu" Alisema bwana Leopold.

"Ndugu zangu wa Kolandoto tupaze sauti unapofanyiwa vitendo vya ukatili wa kijinsia au kuona mtu akifanya vitendo hivyo basi chukua hatua kwa kuripoti tukio katika madawati ya polisi ya kijinsia vilevile unaweza kutua taarifa ya tukio katika ofisi za ustawi wa jamii, serikali za mitaa, vituo vya afya, vituo vya msaada wa kisheria vilivyopo hapa nchini ili kupata huduma kwa wakati msaidie muathirika kuripoti tukio lake ndipo tunaweza kutokomeza vitendo hivi" Aliongeza bwana Leopold.

Naye mratibu wa timu hiyo ya wataalam kutoka Wizara ya Katiba na Sheria bwana George Mollel ambaye ni wakili wa serikali akiongelea haki za Watoto alianza kwa kuelezea kuwa mtoto ni mtu yeyote mwenye umri chini ya miaka kumi na nane na haki za mtoto zinajumuisha haki ya kushirikiana na wazazi wote wawili, kutambuliwa kibinadamu na mahitaji ya msingi ya ulinzi wa mwili, chakula, elimu, huduma ya afya, huku akifafanua sheria zinazofaa kwa ukuaji wa mtoto, haki za kiraia za mtoto, uhuru wa kutokubaguliwa kutokana na jinsia, ulemavu, dini, kabila au sifa nyingine.

Wakili Mollel aliongeza kuwa ulinzi na usalama wa mtoto sio jukumu la maafisa wa ustawi wa jamii peke yao ni jukumu la Taifa kwa ujumla na kwamba hakuna anayeruhusiwa kumdhuru, kumwumiza au kumnyonya mtoto. Yeyote anayejua kwamba kuna mtoto anayeonewa au kutendewa vibaya hana budi kutoa taarifa kuhusu vitendo hivyo kwa; Ustawi wa jamii, Polisi - dawati la jinsia na Watoto, ofisi za serikali za mtaa, taasisi na Mashirika ya kijamii pamoja na kupiga simu namba 116 ya kitaifa isiyo na tozo kwa lengo la kumlinda mtoto.

Aidha bwana Mollea aliwasisitiza wale wote ambao basi wana changamoto binafsi na wamekosa nafasi au hawako huru kueleza changamoto zao katika mikutano hiyo, kufika katika mabanda yanayotoa huduma za kisheria mjini Shinyanga ambapo wataalam wataendelea kuwepo hapo wakitoa huduma hadi tarehe 21 Juni mwaka huu.

Wakitoa salamu za kuhitimisha mikutano hiyo kwa nyakati tofauti wenyeviti wa vijiji hivyo vya Mwamagunguli na Galamba vya kata ya Kolandoto walimshukuru Mhe. Rais kwa kuwaletea kampeni hii huku wakieleza kuwa katika vijiji vyao, ukatili wa kijinsia licha ya kwamba bado upo lakini umepungua baada ya wananchi kuelimishwa kupitia mikutano ya vijiji, ikiwemo wanandoa kutelekeza familia na wanafunzi kuachishwa shule. Na hili limetokana na mikakati iliyowekwa na serikali katika kutoa elimu pamoja na kuwaonesha wananchi ni wapi pa kupeleka malalamiko na kesi zao zinazohusu ukatili wa kijinsia katika jamii, kazi ambayo Kampeni ya Msaada wa Kisheria ya Mama Samia inaendelea kuifanya hivi sasa.

Mama Samia Legal Aid Kampeni inayoongozwa na kauli mbiu inayosema "Msaada wa kisheria kwa haki, usawa, amani na maendeleo" imedhamiria kuongeza wigo wa ufikiwaji haki kwa wananchi, hususan walio vijijini na ambao hawawezi kumudu gharama za mawakili. Kampeni hii pia imekuwa msingi mzuri wa kujenga uelewa wa wananchi kuhusu haki zao za kikatiba na kisheria; jambo ambalo ni muhimu katika kulinda na kukuza haki za binadamu nchini. Hii ni kampeni ya miaka mitatu yenye lengo la kufikia mikoa yote nchini huku ikitarajiwa kuhitimishwa mwaka 2026.



Afisa ustawi wa jamii wa Hospitali ya Mkoa wa Shinyanga ambaye ni mmoja wa wataalam wanaoetekeleza Mama Samia Legal Aid Campaign (MSLAC) mkoani Shinyanga, bwana Leopold Hamza akizungumza na wananchi.



Mmoja wa wananchi akifuatilia kwa makini elimu inayotolewa na wataalam wanaoendesha kampeni ya MSLAC walipofika kijijini Galamba.



Sehemu ya wananchi wa Kijiji cha Galamba wakimsikiliza Wakili Msomi George Mollel wakati akitoa elimu ya shera kuhusu mirathi kwa wananchi hao.

# "KAHAMA INAONGOZA KWA MIGOGORO YA ARDHI SHINYANGA" - MNDEME

**Na Lusajo Mwakabuku – WKS Shinyanga**



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga Bi. Christina Mdeme na Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro wakifurahia jambo mara baada ya Waziri Ndumbaro kuwasili ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga leo 15/06/2023.

Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga Bi. Christina Mdeme ameitaja wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga kuwa kinara wa migogoro ya ardhi inayopelekea wakazi wa wilaya hiyo kupoteza muda mwingi na nguvu kazi katika mahakama na mabaraza ya ardhi kutafuta muafaka ambapo kwa baadhi ya maeneo ya wilaya hiyo, migogoro ya ardhi imesababisha madhara makubwa.

Kauli hiyo imetolewa na Mkuu wa Mkoa leo tarehe 15/06/2023 wakati akimkaribisha Waziri wa Katiba na Sheria Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro aliyefika mkoani hapo kwa lengo la kukagua utekelezaji wa Mama Samia Legal Aid Campaign pamoja nakutoa huduma kwa wananchi kupitia kampeni hiyo iliyozinduliwa rasmi mkoani hapa Juni 11 mwaka huu na itaendelea mpaka tarehe 21/06/2023.

Mheshimiwa Mndeme alianza kwa kumshukuru Mhe. Ndumbaro kwanza kwa kumteua yeye kuwa Mgeni Rasmi katika ufunguzi wa Kampeni hii mkoani Shinyanga lakini pia akaelezea kufarijika kwa jinsi timu za utangulizi zilivyoweza kufanya kazi kwa kushirikiana na uongozi wa mkoa katika kufanikisha utekelezaji wa kampeni hii. Baada ya salamu hizo, ndipo Mkuu wa Mkoa huyo akaeleza kufurahishwa kwake na ujio wa hii kampeni hasa katikamaeneo ambayo yamekuwa yakiongoza kwa migogoro.

"Katika mkoa huu wa Shinyanga, Wilaya ya Kahama ndio wilaya inayoongoza kwa migogoro ya ardhi, na hili linatoka na uwepo wa watumishi waliopewa dhamana ya kuhudumia wananchi ambao wamekosa maadili na kushindwa kusimamia haki suala linalosababisha migogoro isiyoisha" Alisema Mndeme.

Mndeme aliongeza kwamba kumekuwa na ucheleweshwaji mkubwa wa huduma za utoaji haki unaopelekea baadhi ya kesi kuchukua muda mrefu huku matukio ya kudhulumiana nyumba, mashamba na viwanja yakiendelea kuongezeka katika maeneo mbalimbali wilayani Kahama na akamuomba Waziri Ndumbaro na timu yake kuangalia kwa jicho la kipekee wilaya hiyo kwa lengo la kuwapunguzia wanachi kero hizo.

Akifafanua zaidi kuhusu migogoro hiyo, Mhe. Mndeme alisema maadili mabovu ya watumishi yamesababisha utolewaji wa hukumu usiozingatia haki kiasi viongozi wa mkoa wakalazimika kuingilia kati kwa baadhi ya kesi baada ya kuona kuwa hukumu zinatolewa bila kuzingatia haki lengo likiwa ni kuwafaidishsha wale wenye vipato vikubwa na kuwakandamiza wanyonge.

"Imefikia wakati sisi viongozi wa Mkoa tunalazimika kuingilia kati baada ya kuona watu wakipatiwa hukumu ambazo hazijakidhi vigezo zinazopelekea wanyonge kuvunjiwa mali zao hasa nyumba wanazoishi na wao kushindwa kupambana kwa kuwa wanaoshindana nao wana uwezo mkubwa kifedha na wao hawawezi kumudu gharama za kuwapata watu wa kuwatetea, ndio maana nasema kampeni hii imekuja wakati muafaka kwani sasa wanyonge wa mkoani kwangu wanapata sauti" Aliongezea Mndeme.



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga Bi. Christina Mdeme akimwelezea Mhe. Ndumbaro na wageni alioongozana nao jinsi Mama Samia Legal Aid Campaign inavyoendelea kutekelezwa Shinyanga.

Akiongelea masuala ya mmomonyoko wa maadili kwa wananchi, Mndeme ameitaka timu ya wataalam wakati wanatoa elimu wasisitize pia suala la kulinda maadili kwani masuala ya ubakaji na ulawiti bado yapo katika jamii yaw ana Shinyanga na pia akatumia nafasi hiyo kumuomba Mhe. Waziri na watu wake kuangalia upya hizi sheria ambazo zinampa dhamana mbakaji au mtu anayelawiti akisisitiza kuwa hii ni kama tabia na mbakaji si mtu anayefaa kuchanganywa na jamii kwani hizi dhamana zinawapa nafasi za wao kujaribu tena vitendo hivyo na hivyo kuwatia hatarini watu wanaowazunguka.

Wataalam wanaoendesha kampeni ya msaada wa kisheria ya Mama Samia inayofahamika kama Mama Samia Legal Aid Campaign wapo Mkoani Shinyanga kwa siku Kumi na baada ya hapo wataelekea Mkoani Ruvuma kuendelea na kampeni hiyo.



CS CamScanner

# NDUMBARO AONYA UTOAJI MIKOPO BILA MWENZA KUJUA



Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dk. Damas Ndumbaro akitoa elimu pamoja na kutatua migogoro mbalimbali ya kisheria kwa wananchi wa Maganzo, wilayani Kishapu mkoani Shinyanga.

## Na Mwandishi wetu

Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dk. Damas Ndumbaro (Mb) ameziagiza taasisi za mikopo (microfinance) kuhakikisha mwenza wa wanayempa mkopo nae amesaini makubaliano ya kuchukua mkopo huo ili kupunguza ama kuondoa migogoro inayozalishwa katika familia kutokana na mikopo hiyo.

Waziri Ndumbaro aliyasema hayo mkoani Shinyanga tarehe 15 Jumi, 2023 wakati akitoa elimu pamoja na kutatua migogoro mbalimbali ya kisheria kwa wananchi wa Maganzo, wilayani Kishapu ikiwa ni siku ya tano ya kampeni inayoendelea ya kitaifa ya msaada wa kisheria ya Mama Samia iliyolenga kutoa elimu na msaada wa kisheria bure kwa wananchi hasa wa vijijini ambao hawawezi kumudu gharama za mawakili.

Waziri Ndumbaro alisema kuwa kumekuwa na ongezeko la migogoro katika familia kufuatia mmoja wa wanandoa kuchukua mkopo bila mwenza wake kujua hali inayopelekea kuchukuliwa kwa thamani za nyumbani au hata nyumba kuuzwa pindi mkopo huo unaposhindwa kurejeshwa.

"Kwa mujibu wa sheria ya ndoa. Wewe ambae unatoa mkopo lazima uhakikishe mwenza wa huyo unayempa mkopo nae amesaini. Ukimpa mke peke yake mume hajui, au ukampa mkopo mume peke yake bila mkewe kujua imekula kwako" Alisema Mhe. Ndumbaro.



Mwananchi akiuliza swali kwa Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dk. Damas Ndumbaro mara baada ya Mhe. Waziri kutoa elimu kwa wananchi hao.

Ndumbaro aliendelea kuwaelimisha wananchi hao kuwa itakapotokea kuna taasisi imemkopesha mwenza wako bila wewe kujua na kusaini basi una haki ya kukataa wasizuie au kuuza mali ya familia kwani sheria inazitaka taasisi hizo kuhakikisha nume au mke ameridhia mkopo huo kuchukuliwa.

"Na mara nyingi taasisi hizo zinazotoa mikopo kwa siri ni zile taasisi zinazotoa mikopo "nyonya damu" mikopo ambayo huwa ni vigezo vigumu na riba kubwa lengo likiwa si kumsaidia mtanzania wa kawaida bali kumuingiza katika matatizo zaidi" Aliongeza Waziri Ndumbaro.

Akijibu baadhi ya maswali yaliyoulizwa na Wananchi likiwemo swala la kama mtoto ana haki ya kuzuia mali ya mzazi wake isiuzwe kwani pale mzazi anapoamua kuuza nyumba au mali nyingine yeyote anayomiliki, Waziri Ndumbaro alisema mtoto hana haki yeyote ya kumzuia baba yake au mama yake kuuza mali aliyoichuma mwenyewe, mwenye haki ya kupinga hilo ni mke au mme katika familia.

Pamoja na mazungumzo hayo Ndumbaro aliwataka wananchi wa Maganzo kuitumia vyema fursa hiyo ya wataalam wa kisheria walioletwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kushughulikia masuala yao ya kisheria bure ili waweze kuishi kwa amani, usawa na waweze kujipatia maendeleo.



Mwalimu Theresia Josephat aliyewabaini watoto watoro sugu na baada ya kuwafuatilia, na kubaini kuwa watoto hao walikuwa wakijificha kwenye vichaka na majumba mabovu walikuwa wanajifundisha na vitendo vya ulawiti.



CamScanner



Waziri wa Katiba na Sheria, Dk. Damas Ndumbaro (kulia) akimsikiliza mkazi wa kijiji cha Wishiteleja, wilayani Kishapu mkoani Shinyanga, Bibi Limi Jakala mwenye umri wa miaka 100 akimuelezea namna mwanae alivyotaka kumnyanga kufuatia mgogoro wa ardhi katika familia hiyo. Waziri Ndumbaro alienda kumsikiliza bibi huyo ikiwa ni sehemu ya kampeni inayoendelea ya kitaifa ya msaada wa kisheria ya Mama Samia iliyolenga kutoa msaada wa kisheria bure kwa wananchi. (Picha na Mpigapicha Wetu)

# MSAADA WA KISHERIA KUTOLEWA BURE KILA JUMAMOSI YA MWISHO WA MWEZI

**Na George Mwakyembe**

Waziri wa Katiba na Sheria, Mhe. Dk. Damas Ndumbaro (Mb) amewaagiza Wakuu wa Mikoa pamoja na Wakuu wa Wilaya nchini kutenga kila Jumamosi ya mwisho mwezi kutoa elimu na kutatua migogoro ya kisheria bure kwa wananchi.

Waziri Ndumbaro aliyasema hayo jana mkoani Shinyanga wakati akizungumza na wananchi wa Maganzo, wilayani Kishapu ikiwa ni siku ya tano ya kampeni inayoendelea ya kitaifa ya msaada wa kisheria ya Mama Samia mkoani huko iliyolenga kutoa elimu na msaada wa kisheria bure kwa wananchi hasa wa vijijini ambao hawawezi kumudu gharama za mawakili.

Waziri Ndumbaro alisema huduma ya msaada wa kisheria kuwafikia wananchi bure ni mapenzi makubwa ya Rais Samia Suluhu Hassan kwa wananchi wa Tanzania na hasa wanyonge wasio na uwezo wa kulipa gharama za mawakili.

"Toka Juni 11 wataalam wetu wapo katika Wilaya mbalimbali za Mkoa wa Shinyanga na watakuwa hapa kwa siku 10 toka tarehe hiyo. Sio tuu wanawapa elimu lakini pia wanasikiliza changamoto zenu na kuzitatua. Migogoro mingi imesuluhishwa.

Tutaendelea kutatua migogoro hii ndani ya kipindi hiki cha siku kumi lakini mpango huu utakuwa endelevu. Katika kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi kuanzia mwezi Julai, tutaendelea na huduma hii, elimu na utatuzi wa migogoro ya kisheria bure kabisa," alisema huku akitoa wito kwa wananchi kujitokeza kupata msaada wa utatuzi wa migogoro inayowasumbua ili jamii iwe na amani.

Dk. Ndumbrao pia alitoa onyo kwa viongozi waliopewa dhamana ya kuwatumikia wananchi kuhakikisha wanatenda haki ili kuondoa migogoro katika jamii husika, huku akisema hatua kali zitachukuliwa kwa wataobainika kuwa chanzo cha migogoro.

"Katika kampeni hii pia pale penye matatizo ya kimfumo au ya watendaji tunakwenda kurekebisha. Watendaji wabovu hakuna namna tutawachomoa. Watendaji ambao kazi yao ni kudhulumu haki za wananchi, hatutawaacha salama. Na tutaanza na Mkoa wa Shinya, tutaondoka nao," alisisitiza Waziri Ndumbaro.

Awali, Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Bi. Christina Mndeme alibainisha kuwa moja ya changamotokubwa katika mkoa huo inayopelekea wananchi wengi kukosa haki zao ni ukosefu wa maadili kwa baadhi ya watu waliopewa dhamana ya kutoa haki kwa wananchi.

"Kupitia Kampeni hii ya msaada wa kisheria ya Mama Samia watu watakwenda kupata haki zao. Na wale waliokuwa hawajui wapi pakwenda kupata haki zao watapa msaada kutoka kwa wataalam waliopo," alisema Mkuu huyo wa Mkoa.



CS CamScanner



Waziri wa Katiba na Sheria nchini Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro akimueleza Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga dhima ya utekelezaji wa Mama Samia Legal Aid Campaign.

# "TUMEAGIZWA KUFANYA LEGAL ENGINEERING"

## NDUMBARO

**Na Lusajo Mwakabuku – Shinyanga**

Waziri wa Katiba na Sheria nchini Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro amesema utekelezaji wa Mama Samia Legal Aid Campaign unatokana na maono pamoja maagizo mbalimbali ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania likiwemo agizo alilolitoa wakati akizindua "Lawyers Bar Association" la kuitaka Wizara kufanya Legal Engeneering akimaanisha wizara kujenga, kuboresha na kurahisisha mifumo itakayosaidia upatikanaji wa haki na amani kwa kupitia msaada wa kisheria.

Waziri Ndumbaro aliyasema hayo alipokuwa katika ziara ya kikazi mkoani Shinyanga kwa lengo la kukagua utekelezaji wa kampeni ya huduma ya msaada wa kisheria inayoendelea katika wilaya na halmashauri mbalimbali mkoani Shinyanga ambapo inatarajiwa kuhitimishwa kwa awamu ya kwanza tarehe 21 Juni mwaka huu.

"Kampeni hii ambayo imepewa heshima kubwa kwa kupewa jina la kiongozi wetu mkuu wa nchi inatokana na ilani ya Chama Cha Mapinduzi ambayo imeagiza waananchi wapate elimu ya sheria na msaada wa sheria katika kutatua changamoto mbalimbali wanazozikabili, lakini pia kampeni hii ni maelekezo ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan ambapo mara nyingi amekuwa akiongelea kuwasaidia wanyonge kupata haki ikiwemo agizondipo wizara ikaja na kampeni hii hivyo niwapongeze Mkoa wa Shinyanga kwa kuendelea kutoa huduma ya msaada wa kisheria ", amesema Waziri Ndumbaro.

"Lengo mahususi la kampeni hii ni kuhakikisha kuwa kuna haki, amani, usawa na maendelea katika nchi, programu yetu itawafikia nchi nzima bara na visiwa na niwahakikishie kuwa watendaji wabovu hakuna namna tutawachomoa, watendaji ambao kazi yao ni kuzurumu haki za wananchi hatutawaacha salama na tutaanza na mkoa huu wa Shinyanga", ameongeza Waziri Ndumbaro.

Aidha Waziri Damas Ndumbaro ametatua mgogoro wa kifamilia uliodumu kwa miaka nane katika kijiji cha Wishiteleja ambapo alielekeza hatua za kisheria kuchukuliwa dhidi ya mtuhumiwa wa kata ya Mondo wilayani Kishapu mkoani humo na pia alifanikiwa kufanya mkutano wa hadhara na wananchi wa kata ya Maganzo ambapo kupitia mkutano huo ametoa elimu na kusikiliza migogoro iliyokuwa ikiwakabili wakazi wa eneo hilo.

Awali akitoa taarifa ya utekelezaji wa Kampeni ya Mama Samia legal Aid Campaign ngazi ya mkoa, Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga Mhe. Christina Mndeme amesema kampeni hiyo imekuwa msaada mkubwa katika kutatua migogoro ya iliyokuwa ikitokana na ukosefu wa elimu ya masuala ya sheria na kusema miongoni mwa sababu zinazopelekea migogoro ni tabia ya baadhi ya watumishi kukosa maadili ya misingi na taratibu ya kazi yao.

"Mara baada ya kuanzishwa kwa kampeni hii ya msaada wa kisheria imekuwa ni mkombozi mkubwa kwenye jamii kwa kupunguza migogoro ya ardhi, uridhi na mambo mengine yanayohusiana na sheria Kupitia kampeni hii dhuruma waliokuwa wakikumbana nayo wananchi na kukosa haki zao sasa inakwenda kuisha kwani mpaka sasa malalamiko yamepungua, Tunamshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kutuletea kampeni hii ndani ya mkoa tunaahidi kuendelea kutoa ushirikiano ili malengo ambayo serikali imejiwekea yaweze kufikiwa", amesema RC Mndeme.

Pia Mndeme amemuomba Waziri wa Katiba na Sheria kupitia upya vifungu vya sheria vinavyotoa dhamana kwa wanaokutwa na hatia ya kujihusisha na vitendo vya ubakaji na ulawiti kwani imekuwa chanzo cha kujirudia kwa matukio ya vitendo hivyo.



Waziri wa Katiba na Sheria nchini Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro akiambatata na viongozi wengine wa Katiba na Sheria wakiwa katika ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga.



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga akizungumza na uongozi wa mkoa na wataalam walioambatana na Waziri wa Katiba na Sheria nchini Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro wanaotekeleza Mama Samia Legal Aid Campaign.



CamScanner

# **Habari Picha** Shinyanga






Bi. Christina Mndeme
Mkuu wa Mkoa Shinyanga



Bi. Pauline Gekul
NW wa Katiba na Sheria



Bi. Jane Matinde
Mwakilishi wa Makamu M/kiti

MAMA SAMIA Legal Aid Campaign

**Uzinduzi**
11 Juni, 2023

CamScanner



Viongozi wa meza kuu wakipita kukagua kazi zilizokuwa zikiendelea katika mabanda ya kutolea huduma siku ya ufunguzi wa utekelezaji wa Mama Samia Legal Aid Campaign Mkoani Shinyanga




CamScanner

Waziri wa katiba na Sheria Mhe. Dkt. Damas Ndumbaro akipata maelezo kutoka kwa mratibu wa kampeni ya MSLAC na baadae kutatua mgogoro wa kifamilia uliodumu kwa miaka nane katika kijiji cha Wishiteleja kata ya Mondo wilayani Kishapu mkoani Shinyanga



MAMA SAMIA Legal Aid Campaign

CamScanner

Mjane bibi Fatuma Maganga akiongea na wataalam kutoka Mama Samia Legal Aid Campaign waliofika kushuhudia ubomoaji wa eneo ambalo mama huyu alivamiwa na licha ya Mahakama kutoa hukumu ya mvamizi kuondoka bado mvamizi huyo aliendelea kumiliki eneo hilo mpaka ilipokuja MSLAC.








MAMA SAMIA Legal Aid Campaign

CamScanner